# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHUO KIKUU CHA DODOMA

TANZANIA
Registered this 6th
day of August 20 20
Asst. Registrar of Cooperative Societies

SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY

UDOM SACCOS
*Pamoja Tujenge Uchumi Wetu*

## (UDOM SACCOS LTD)
## NA. YA USAJILI: DOR 715

# SERA YA UWEKEZAJI

**Imetengenezwa Chini ya Kanuni ya 49 ya Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) 2019**

**Imeandaliwa na Bodi ya UDOM SACCOS LTD**
**S.L. P 2765**
**Barua Pepe: udomsaccosltd@gmail.com**
**DODOMA- TANZANIA**

**TOLEO NA: 2020**

# YALIYOMO

*DIBAJI* .......... 2
SEHEMU YA KWANZA .......... 2
1.0 UTANGULIZI .......... 2
1.1 Historia fupi ya Chama .......... 2
1.2 Wigo na Madhumuni ya Sera .......... 3
1.2.1 Madhumuni ya Sera ya uwekezaji .......... 3
SEHEMU YA PILI .......... 3
2.0 MAENEO AMBAYO CHAMA KINATAKIWA KUWEKEZA .......... 3
2.1 Maeneo ambayo chama kinaweza kuwekeza .......... 3
2.2 Mambo ya kuzingatia kabla ya uwekezaji .......... 4
2.3 Muda wa kuiva wa uwekezaji .......... 5
SEHEMU TATU .......... 5
3.0 HATARI ZINAZOWEZA KUJITOKEZA WAKATI WA UWEKEZAJI .......... 5
SEHEMU YA NNE .......... 6
4.0 MAMLAKA YA KUFANYA UWEKEZAJI NA MGAWANYO WA MAJUKUMU .......... 6
4.1 Mamlaka ya Uwekezaji .......... 6
4.1.2 Mkutano Mkuu wa mwaka wa Chama .......... 6
4.1.3. Bodi ya chama .......... 6
4.2 Mgawanyo wa Majukumu .......... 6
4.2.1 Majukumu ya Bodi ya Chama .......... 6
4.2.2 Majukumu ya Menejimenti .......... 7
SEHEMU YA TANO .......... 7
5.0 UTOAJI WA TAARIFA ZA UWEKEZAJI .......... 7
HITIMISHO .......... 8

## *DIBAJI*

*Sera hii ya uwekezaji ya UDOM SACCOS Ltd imeandaliwa na Bodi ya chama kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013, Sheria ya Huduma ndogo za fedha Na. 10 ya mwaka 2018 na Kanuni ya 49 za Huduma ndogo za fedha (SACCOS) za mwaka 2019. Sera hii inatoa mwongozo sahihi wa uwekezaji wa chama kuwekeza katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia kifungu cha 74 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na Kanuni ya (49 - 50) ya Kanuni za Huduma ndogo za Fedha za mwaka 2019.*

*Bodi na menejimenti wakati wote itawekeza kwa maslahi mapana ya Wanachama na Chama kwa kuzingatia sera hii.*

*Sera hii imejumuisha Sehemu tano, **Sehemu ya kwanza** ni utangulizi, **sehemu ya pili ni** umuhimu wa uwekezaji, **sehemu ya tatu** ni maeneo ya uwekezaji (Investment destination), **sehemu ya nne** ni Kuiva kwa uwekezaji na hatari zinazoweza kujitokeza wakati wa uwekezaji (Investment maturity and Risks) na **Sehemu ya tano** ni Utoaji wa taarifa za uwekezaji kwa Bodi ya Chama.*

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Historia fupi ya Chama

UDOM SACCOS Ltd ni Chama cha akiba na mikopo kilichoandikishwa tarehe 05 Januari 2011 na kupewa nambari ya usajili DOR 715. Mfungamano wa Wanachama wa UDOM SACCOS Ltd ni Watumishi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Watendaji wa UDOM SACCOS Ltd na Waliokuwa Watumishi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na kuhamia katika Taasisi na Mamlaka nyingine za Serikali. Eneo la shughuli za UDOM SACCOS Ltd ni katika Chuo Kikuu cha Dodoma ndani ya Jiji la Dodoma.

## 1.2 Mawanda ya Sera

Sera hiii inatoa mwongozo wa kisheria na uwazi katika uwekezaji wa aina mbalimbali utakaofanywa na Chama kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 ya mwaka 2018 na Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) ya mwaka 2019.

Sera hii itatumika wakati wote kama mwongozo wa kuzingatiwa wakati wa kufanya maamuzi ya uwekezaji (Investment decisions) kwa maslahi mapana ya Wanachama na Chama.

## 1.3 Madhumuni ya Sera ya Uwekezaji

i. Kuainisha majukumu ya pande zote zitakazohusika katika Uwekezaji.
ii. Kuweka utaratibu utakaozingatiwa katika mchakato wa maamuzi ya uwekezaji.
iii. Kuweka uelewa wa pamoja kwa wahusika wote juu ya malengo ya uwekezaji.
iv. Kutoa mwongozo na ukomo wa uwekezaji utakaofanywa na Chama.
v. Kuweka mwongozo wa kufanya tathimini ya uwekezaji
vi. Kupima kama uwekezaji uliofanyika unasimamiwa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAENEO AMBAYO CHAMA KINATAKIWA KUWEKEZA

Shughuli kuu ya chama ni kupokea akiba za wanachama na kutoa mikopo kwa Wanachama wake. Hivyo kipaumbele cha uwekezaji wa fedha za Chama utakuwa ni kutoa mikopo kwa Wanachama wake.

## 2.1 Maeneo ambayo Chama Kinaweza Kuwekeza

Chama kitawekeza kwenye maeneo mengine endapo Chama kitakuwa na ukwasi toshelevu, hivyo Chama kinaweza kuwekeza katika maeneo yafuatayo:.

i. Kuwekeza fedha katika benki kama Amana za muda maalumu (FDR).

ii. Kuwekeza kwenye taasisi nyingine za kifedha kama vile ununuzi wa vipande UTT au hisa katika kampuni zinazofanya vizuri katika soko la Hisa (DSE).
iii. Kuwekeza katika dhamana za Serikali (Government Securities).
iv. Kuwekeza kwenye SACCOS na Vyama vya Ushirika vya upili (second tier or secondary cooperative societies)
v. Kuwekeza katika mali zisizozalisha (Non-Earning assets) kama vifaa, majengo na ardhi ambapo;
    a) Chama kitawekeza katika mali zisizozalisha (non- earning assets/property/Equipment) kwa kiwango kisichozidi asilimia 10 % ya mali zote za chama.
    b) Uwekezaji katika ardhi na majengo hautazidi asilimia 5% ya mali zote za chama.

Aidha, Chama kinaweza kuwekeza katika mradi wowote ambao utaruhusiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

## 2.2 Mambo ya Kuzingatia Kabla ya Uwekezaji

Kabla ya kufanya maamuzi ya kuwekeza, Chama kitafanya upembuzi wa kina kikizingatia mahitaji na hali halisi ya ukwasi na vipindi vya mahitaji makubwa ya mikopo kwa Wanachama. Chama kitakapo hitaji kuwekeza, kitapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:-

i. Kufanya tathimini ya kina juu ya mahitaji na uwezo wa kifedha wa Chama.
ii. Muda wa kuiva kwa uwekezaji (Investment Maturity).
iii. Mapato tarajiwa toka kwenye uwekezaji husika (Return on investment).
iv. Vihatarishi kwenye uwekezaji (Investment risks).
v. Utendaji wa taasisi/kampuni husika (Performance trend analysis).
vi. Sera za uwekezaji za Sekta husika.
vii. Historia ya Taasisi husika.
viii. Gharama za uwekezaji.
ix. Na mambo mengine kulingana na mazingira husika.

## 2.3 Muda wa Kuiva kwa Uwekezaji

Chama kitaweza kuwekeza katika maeneo ambayo muda wa uwekezaji utazingatia miongozo itakayotolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 NAMNA YA KUPUNGUZA VIHATARISHI

Chama kinatakiwa kufanya uwekezaji kwenye maeneo tofauti tofauti (Portfolio diversification) ili kupunguza hatari ya kupata hasara kubwa. Hivyo, uwekezaji utatakiwa kuzingatia mambo matatu ambayo ni usalama, ukwasi na faida tarajiwa. Usalama wa uwekezaji utakuwa ndio lengo kuu la mpango wa uwekezaji.

Ili kupunguza hatari katika uwekezaji Chama kitatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

i. Chama hakitaweka fedha katika benki moja au taasisi moja ya kifedha kwa kiwango kinachozidi asilimia 25% ya mtaji tete wa Chama kwa ajili ya kufanya mtawanyo wa vihatarishi (diversification of risks or risks spread).

ii. Chama kitatatikiwa kuwekeza kwenye maeneo salama yaliyotajwa kwenye Sera hii katika sehemu ya pili.

iii. Chama kinatakiwa kufanya uwekezaji kwenye dhamana za muda mfupi na mrefu, masoko ya fedha (money market) na kudhibiti muda wa uwekezaji.

## SEHEMU YA NNE

# 4.0 MAMLAKA YA KUFANYA UWEKEZAJI NA MGAWANYO WA MAJUKUMU

## 4.1 Mamlaka ya Uwekezaji

### 4.1.2 Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama

Baada ya Bodi kupeleka mapendekezo, Mkutano Mkuu wa mwaka wa Chama utakuwa na mamlaka ya kupitisha aina yoyote ya uwekezaji unaotakiwa kufanywa na Chama. Aidha, baada ya Mkutano Mkuu kupitisha, Chama kitatakiwa kupeleka maombi ya kuidhinishiwa uwekezaji huo kwa Mrajis.

### 4.1.3. Bodi ya Chama

Bodi ya Chama itakasimishwa kufanya uwekezaji kwa niaba ya Wanachama. Hivyo, Bodi itapaswa kuzingatia maazimio na maelekezo ya Mkutano Mkuu wa Chama.

## 4.2 Mgawanyo wa Majukumu

### 4.2.1 Majukumu ya Bodi ya Chama

Bodi ya Chama itakuwa na jukumu la kuelekeza na kusimamia uwekezaji wa Chama. Bodi itatekeleza majukumu yake kwa maslahi ya Chama kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Masharti ya Chama. Majukumu ya Bodi kwenye utekelezaji wa Sera hii yatakuwa kama ifuatavyo:

i. Kufanya tathimini ya vihatarishi katika uwekezaji na mipaka ya uwekezaji na kutoa taarifa kwa pande zote zinazohusika.
ii. Kuisimamia Menejimenti ya Chama katika uendeshaji wa mradi.
iii. Kuandaa taarifa ya maendeleo ya uwekezaji na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Wanachama.
iv. Kujadili hali ya mwenendo wa uwekezaji kwenye vikao vya Bodi vya kila robo mwaka.
v. Kushauri Wanachama juu ya fursa nyingine za uwekezaji.

### 4.2.2 Majukumu ya Menejimenti

Menejimenti ya Chama itawajibika kwa Bodi ya Chama na itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kutekeleza maamuzi ya uwekezaji yaliyofikiwa na Bodi.
ii. Utunzaji wa kumbukumbu na uandaaji wa taarifa za fedha za uwekezaji na kuziwasilisha kwa Bodi.
iii. Kupendekeza kwa Bodi fursa zozote za uwekezaji kulingana na mwenendo wa uchumi uliopo.
iv. Kufuatilia na kutoa taarifa kwa Bodi juu ya maendeleo na shughuli za uwekezaji mara kwa mara.
v. Kushauri Bodi kufanya mapitio na maboresho ya Sera hii.
vi. Kuwasilisha taarifa kwa Bodi juu ya mabadiliko makubwa ambayo yanaweza kuathiri ufikiaji wa malengo ya uwekezaji Wa Chama.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 UTOAJI WA TAARIFA ZA UWEKEZAJI

Menejimenti ya Chama itatakiwa kutoa taarifa ya uwekezaji kwa Bodi ya Chama angalau kila mwezi au isizidi robo mwaka. Taarifa hiyo itaainisha mambo yafuatayo;

i. Aina zote za uwekezaji uliofanywa na Chama.
ii. Riba halisi ya kila uwekezaji mpaka siku taarifa hiyo inapotolewa.
iii. Tarehe ya kuiva kwa kila uwekezaji na taarifa nyingine zinazohusiana na uwekezaji.
iv. Shughuli za uwekezaji za kila mwezi kama vile kununua na kuuza, na riba iliyorejeshwa.
v. Malinganisho ya kwenye vitabu (book value) na malinganisho ya soko kwa wakati husika (current market value).
vi. Na taarifa nyingine muhimu kama zipo.

## HITIMISHO

Sera hii ya Uwekezaji wa Chama itafanyiwa marekebisho/mapitio au mabadiliko angalau kila mwaka ili kuboresha jambo/mambo yatakayo onekana yanahitajika kuboreshwa kwa maslahi mapana ya Chama na Wanachama kadiri Bodi ya uongozi na Wanachama watakavyoona inafaa.

Sera hii imetayarishwa na kupitishwa Bodi ya UDOM SACCOS Ltd kwa niaba ya wanachama; katika kikao kilichofanyika tarehe ..05.. Mwezi ..04.., mwaka ..2020..

*Mrajis wa Vyama vya Ushirika*

Tarehe 05/08/2020

TANZANIA
Registered this 5th
day of August 2020
Asst. Registrar of Cooperative Societies